**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE HAFLA YA KUPOKEA GAWIO KUTOKA BENKI YA NMB

**Ukumbi wa Kambarage,**
**DODOMA**
**Juni 15, 2022**

**Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb.), Waziri wa Fedha na Mipango;**

**Mhe. Othman Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango;**

**Mhe. Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;**

**Mhe. Jerry Silaa (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yako waliopo;**

**Bw. Emmanuel Tutuba, Katibu Mkuu - Wizara ya Fedha na Mipango;**

**Bw. Mgonya Benedicto, Msajili wa Hazina;**

**Prof. Florens Luoga, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania;**

**Dkt. Edwin Mhede, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya NMB;**

**Mama Ruth Zaipuna, Afisa Mtendaji Mkuu Benki ya NMB;**

**Viongozi wote mliopo hapa;**

**Menejimenti na Watumishi wa Benki ya NMB; Msajili wa Hazina na Wizara ya Fedha na Mipango;**

**Waandishi wa Habari;**

**Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana.**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…**

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kufika hapa kushiriki Hafla hii muhimu ya kupokea Gawio la Serikali kutoka Benki ya NMB kwa mwaka 2021. Natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango, pamoja na Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya Benki ya NMB, kwa kunipa heshima ya kuwa Mgeni Rasmi katika tukio hili muhimu ambalo linaashiria kuwa, Benki imeendelea kukua na kufanya vizuri kiutendaji.

Serikali, kwa niaba ya wananchi, inafurahia sana juhudi mnazozifanya kuchangia maendeleo ya Taifa letu. Ninakupongeza sana Dkt. Edwin Mhede pamoja na wajumbe wote wa Bodi ya Wakurugenzi kwa kusimamia vema NMB. Aidha, kwa namna ya pekee ninampongeza na kukushukuru wewe binafsi Mama Ruth Zaipuna, Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Menejimenti, pamoja na Watumishi wote wa Benki ya NMB kwa utendaji wenye tija ambao umeiwezesha Benki kupata faida, kulipa kodi stahiki pamoja na kutoa gawio nono kwa Serikali na Wanahisa wengine. Serikali pamoja na Wanahisa wote wa Benki ya NMB tunajivunia mafanikio haya

makubwa na ya mfano ambayo kwakweli yanatia moyo na kutoa hamasa. **Asanteni na hongereni sana.**

**Pili,** naomba kuwasilisha salamu za pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mafanikio makubwa mnayoendelea kuyapata. Pamoja na salamu, Mheshimiwa Rais anasisitiza muendelee kuwa wabunifu katika kazi yenu muhimu ya kufikisha huduma bora za kifedha kwa wananchi na hasa wale ambao bado hawajafikiwa na huduma hizo, hasa vijijini na makundi maalum hususan wanawake na vijana.

Aidha, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anakupongeza sana Mama Ruth Zaipuna, kwa kutunukiwa **Tuzo ya Afisa Mtendaji Mkuu Bora wa Benki Afrika kwa Mwaka 2022.** Tuzo hii inadhihirisha ubunifu wako, kujitoa kwako katika kazi na uongozi wako madhubuti unaozingatia kutoa huduma bora kwa wateja. Hali kadhalika, tuzo hii pia inadhihirisha kuwa kina Mama wenye sifa, wakipewa fursa ya kuongoza, wanafanya kweli! Nami naungana na Mheshimiwa Rais kukupongeza kwa dhati. **Hongera sana Mama Ruth Zaipuna.**

***Waheshimiwa Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Itakumbukwa mwaka jana wakati napokea gawio kutoka benki ya NMB kwenye ukumbi huu, niliwaagiza Mwenyekiti wa Bodi pamoja na Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki yetu hii ya NMB kuhakikisha wanaongeza gawio kwa Serikali na kwa wanahisa wengine. Nafurahi sana kuona mmetekeleza na mmeleta gawio nono kabisa. Ni jambo la kujivunia kuona kuwa Serikali ambayo ina umiliki wa asilimia 31.8 ya hisa za Benki ya NMB, inapata kiasi cha **Shilingi bilioni 30.7** kama gawio lake. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango uhakikishe fedha hizi zinatumika vizuri kugharamia utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo nchini na kuboresha huduma za jamii ikiwemo Maji, Hospitali, Elimu, Uboreshaji wa Miundombinu ya Barabara, Umeme n.k. ili wenye hisa, ambao ni wananchi wa Tanzania wafurahie uwekezaji wao katika Benki ya NMB.

Vilevile, Serikali na Watanzania tunafurahia na kupongeza jitihada zenu ambazo zilipelekea Benki ya NMB kulipa Serikalini kodi mbalimbali za kiasi cha **Shilingi bilioni 269** katika mwaka 2021 na kupata faida ya Shilingi bilioni 290 baada ya malipo ya kodi, hii ikiwa ni ongezeko la takriban asilimia 41 kutoka faida ya **Shilingi bilioni 206** iliyopatikana mwaka 2020.

***Waheshimiwa Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Serikali inaridhishwa na umahiri wa Benki ya NMB katika kufanya biashara kiushindani. Mmekuwa wabunifu katika kutoa huduma kwa wateja kupitia matumizi ya mifumo ya TEHAMA. Hali hii imesaidia kusogeza huduma za kibenki karibu na watanzania hasa wajasiriamali wadogo. Kwa mfano, ninafahamu kuwa sasa mteja (kama mimi) anaweza kuchukua mkopo wa mpaka laki tano (500,000/=) kwa kutumia simu yake ya Mkononi bila kwenda Benki na bila kuwa na dhamana (MshikoFasta). Hali kadhalika, nilifuatilia Benki ikizindua **NMB Pesa Wakala** owezesha kuwa na Mawakala wengi zaidi sehemu yoyote ya nchi yetu kwani kinachohitajika ni simu zao za Mkononi tu! Huu ni ubunifu mzuri na wa kupongezwa. Lakini kama Mheshimiwa Rais alivyoelekeza, endelezeni ubunifu wenu ili NMB iwe kinara wa ubunifu katika sekta ya fedha nchini (Cutting edge financial innovations).

Sambamba na haya yote, Serikali inaishukuru na kuipongeza Benki ya NMB kwa kuendelea kuchangia maendeleo ya jamii nchini (corporate social responsibility) sambamba na kusaidia ukusanyaji wa mapato ya Serikali; na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato. Napenda kuwasisitiza muendelee kushirikiana na Serikali katika kuongeza fursa za ajira kwa vijana na wanawake na pia kuboresha huduma za kijamii kwenye sekta mbalimbali kama afya na elimu, bila kusahau eneo nyeti la utunzaji wa mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na tabiawatu! Serikali inathamini sana mchango wa NMB. Hata hivyo, niwakumbushe pia mnapoendelea kuwekeza kwenye teknolijia ili kuwafikishia huduma za kifedha watanzania wengi, kwa haraka na kwa unafuu, mhakikishe pia usalama wa mifumo yenu ili kujilinda na wimbi la kuongezeka kwa uhalifu wa kimtandao (*cyber-crime*).

***Waheshimiwa Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Kupitia hafla hii, napenda pia kuipongeza sekta ya benki kwa ujumla kwa kazi nzuri wanayoifanya kuziwezesha kifedha shughuli mbalimbali za kiuchumi hapa nchini. Serikali inafurahi kuona kiwango cha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kimeongezeka kwa kasi kubwa hadi kufikia asilimia 13.4, mwezi Aprili 2022, ukilinganisha na chini ya asilimia 5 kipindi kama hicho mwaka 2021. **Hongera sana** Gavana wa Benki Kuu na timu yako kwa kuisimamia vyema sekta hii nyeti na pia kongole kwa Wakuu wa Taasisi za Fedha nchini. Pamoja na mafanikio haya, napenda kutumia fursa hii kutoa maelekezo yafuatayo:

**Moja**, Benki Kuu, Chama cha Mabenki Tanzania (*Tanzania Bankers Association*) pamoja wa wadau wengine husussan Mwanasheria Mkuu wa

Serikali, kaeni pamoja na kuja na mkakati wa kupunguza kwa haraka zaidi madeni sugu/mikopo chechefu (*non-performing loans (NPL)*). Kiwango cha NPL cha asilimia 8 bado ni cha juu. Athari zake kwenye faida za mabenki na gawio kwa wawekezaji ni kubwa. Zipo taarifa kuwa wapo wakopaji wenye malimbikizo makubwa ya madeni (mikopo chechefu) katika baadhi ya mabenki lakini bado wameendelea kukopeshwa na benki nyingine! Hii ni hatari kwa ustawi wa sekta ya benki. Pamoja na mambo mengine, kuweni macho, mzingatie kanuni na taratibu zinazokubalika katika utoaji wa mikopo na kutumia kikamilifu taarifa za wakopaji (*Credit Reference Bureau*).

**Pili**, suala la riba kubwa za mikopo limekuwa donda ndugu! Kwa mara nyingine ninawataka wadau wote wa sekta ya fedha, wakiongozwa na Benki Kuu ya Tanzania kushirikiana na kuja na tiba ya kushusha riba za mikopo. Kiwango cha sasa cha asilimia 16 bado ni mzigo mkubwa kwa wajasiriamali kuweza kutekeleza ndoto zao za kuwekeza katika Sekta mbalimbali, vijana kujiajiri au kufanya biashara. Ni matumaini yangu kwamba, ndani ya kipindi cha mwaka mmoja magwiji wa sekta ya kibenki mtakuwa mmebuni chanjo ya kuzuia mikopo chechefu.

**Na Tatu**, naomba pia nitumie fursa hii kuwambusha rai ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassana, Rais wa Jmhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati akifungua Jengo la Benki ya CRDB mwezi Machi, mwaka huu 2022 ambapo alizitaka taasisi za kifedha nchini kuiwezesha sekta binafsi ishiriki katika kilimo, hasa cha umwagiliaji ambacho ndiyo kipaumbele cha Serikali kwa mwaka ujao wa fedha. Nawapongeza Benki ya NMB kwa kuanza kutoa kwa mikopo ya riba nafuu ya asilimia 9 kwa wakulima. Hivyo, natoa rai kwa benki nyingine pia kuiga mfano huu na kumuunga mkono Mheshimiwa Rais.

***Waheshimiwa Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Napenda niwahakikishie kuwa Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kuimarisha na kuweka mazingira rafiki na endelevu ya kufanya biashara katika sekta ya fedha na sekta zote. Aidha, Serikali kama mwanahisa itaendelea kutumia huduma za Benki ya NMB kikamilifu ili kuiwezesha kuongeza mapato na hatimaye kuongeza faida zaidi na kulipa kodi na gawio kwa wanahisa kwa kiwango kikubwa zaidi. Hivyo, naendelea kutoa rai kwenu na benki nyingine zote kuendelea kufanya kazi kwa weledi, nidhamu na uadilifu ili kuweza kufikia malengo tuliojiwekea.

Aidha, natambua mchango wa Msajili wa Hazina katika kufuatilia kwa ukaribu suala la utendaji wa mashirika na taasisi zote ambazo Serikali ina hisa, kama

inavyoonekana katika ukuaji wa gawio na mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, wakati Benki ya NMB ikiendelea kutoa gawio nono linaloongezeka mwaka hadi mwaka, bado kuna Mashirika na Taasisi za Umma ambazo uchangiaji wake umekuwa wa kusuasua au kushindwa kabisa kuchangia huku wakitoa visingizio lukuki. Hali hii haipaswi kukubalika! Hivyo, Waziri wa Fedha na Mipango ufuatilie na kuhakikisha kuwa:

**Kwanza**, Mashirika ambayo Serikali ina hisa na hayajaanza kutoa gawio, yaanze kutoa Gawio. Binafsi nimechoka kuimba wimbo huu! Watanzania wanataka faida na tija katika uwekezaji wao katika mashirikia.

**Pili,** Taasisi zinazotakiwa kutoa asilimia 15 ya mapato ghafi kwa mujibu wa sheria zifanye hivyo kikamilifu na kwa wakati.

**Tatu**, Mashirika ambayo yanategemea ruzuku kutoka mfuko mkuu wa Serikali yaje na mikakati madhubuti na inayotekelezeka ya kupunguza utegemezi kwa Serikali. Msajili wa Hazina, uwabane Wakuu wa Taasisi husika watekeleze au kupitia kwa Waziri wa Fedha na Mipango, ulete kwa mamlaka mapendekezo ya kuwawajibisha;

**Nne**, Mashirika yote, Taasisi na Wakala za Serikali zihakikishe zinakidhi matakwa ya Sheria ya Msajili wa Hazina ya kuhakikisha gharama za uendeshaji hazivuki kiwango kilichowekwa kisheria. Hili nalo Msajili wa Hazina na timu yako mlifuatilie kwa kina liishe;

**Na tano**, Bodi na Menejimenti za Mashirika ambayo yamekuwa yanasuasua katika uendeshaji, hayachangii katika Mfuko Mkuu wa Serikali na hayana mchango katika maendeleo ya nchi, nakutaka Waziri wa Fedha na Mipango uwatathmini kama bado wanatosha kwenye nafasi zao na upeleke mapendekezo kwa mamlaka. Na kwenye hili Mheshimiwa Rais, hana utani na mimi binafsi nitafuatilia kwa karibu.

Napenda niwakumbushe kuwa, fedha ambazo Serikali imewekeza kwenye taasisi zenu ni za wananchi, tena wananchi masikini! na Serikali ina wajibu wa kuhakikisha fedha hizo zinazalisha na gawio kutolewa kwa manufaa ya wanahisa ambao ni wananchi.

***Waheshimiwa Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Nimalize hotuba yangu kwa kutoa tena rai kwa Wananchi kuwa na utamaduni wa kuweka fedha zao benki. Nawahakikishia kuwa Benki ya NMB ni mahali salama, panapolipa kuweka fedha zako. Na wale wanaopenda kuwekeza, endeleeni

kununua hisa za NMB ili kuiongezea mtaji na kuendelea kupata huduma zilizo bora na za kiwango. Benki hii ya NMB inakua kwa kasi na inabaki kusimama kuwa ni kielelezo sahihi cha aina ya sekta ya fedha tunayoitaka na pia kielelezo sahihi cha ubinafsishaji wa mashirika ya umma wenye tija.

Kwa mara nyingine tena ninaishukuru Bodi, Menejimenti na wateja wote wa Benki ya NMB kwa kutoa gawio zuri kwa Serikali na wanahisa wenza na nawatakia kazi njema yenye ufanisi.

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**